WISE INVESTOR ACADEMY

# UTT AMIS KWA MTU MWENYE HARAKA

## MWONGOZO MWEPESI WA KUWEKEZA UTT AMIS



MAOMBI ABEL CHAGAMBA

TEL:0713999596

# YALIYOMO

ANGALIZO..........

**UTANGULIZI** .......... 5

**SEHEMU YA KWANZA** ..........

UWEKEZAJI WA PAMOJA NI NINI? ..........

UTTT AMIS NI NINI? ..........

KIPANDE NI NINI?..........

JINSI FAIDA INVYOKUFIKIA KAMA UMEWEKEZA UTT AMIS ..........

1) KUPITIA GAWIO ..........

2) KUPITIA UKUAJI WA MTAJI ..........

FAIDA ZA KUWEKEZA UTT AMIS ..........

MREJESHO WA UWEKEZAJI ..........

**SHEHEMU YA PILI** ..........

MFUKO WA UMOJA..........

MFUKO WA WEKEZA MAISHA ..........

MFUKO WA WATOTO..........

MFUKO WA JIKIMU ..........

MFUKO WA UKWASI ..........

MFUKO WA HATI FUNGANI..........

**SEHEMU YA TATU** ..........

JINSI YA KUANZA KUWEKEZA KWA MARA YA KWANZA ..........

JINSI YA KUKAMILISHA USAJILI ..........

JINSI YA KUUZA VIPANDE VYAKO..........

JUA GHARAMA AMBAZO UNAINGIA WAKATI WA KUWEKEZA ..........

JINSI YA KUTOA FAIDA NA KUBAKIZA MTAJI ..........

MIFUKO YENYE HISA NA MIFUKO ISIYO NA HISA ..........

JE MFUKO UNATOA GAWIO NI BORA KULIKO USITOA GAWIO? ..........

JINSI YA KUJUA BEI YA KIPANDE..........

UWEKEZAJI WA MARA MOJA NA UWEKEZAJI WA MARA KWA MARA..........

MPANGO WA KUWEKEZEWA GAWIO (RE-INVESTMENT) MPANGO BORA WA UTT AMIS. ..........

JINSI YA KUTENGENEZA PENSHENI YAKO. ..........

UTT AMIS VS NYUMBA ..........

MAWASILIANO NA KAMPUNI YA UTT AMIS. ........................................................................
REFERENCES ..........................................................................................................................

# UTANGULIZI

Kama haujawahi kuwekeza kabisa, ngoja nikupe hatua ambazo kila mtu anapitia ili kufikia uhuru wa kifedha (financial freedom)

1) Kupata pesa
2) Kuzalisha pesa
3) Kutunza pesa (protect money)

Kila mtu hapa duniani anapata pesa kwa namna moja au nyingine katika vipindi tofauti vya maisha yake ila changamoto inakuja katika vipengele viwili vya kuzalisha pesa na kutunza (protect) pesa, asikudanganye mtu ya kuwa unaweza kufikia uhuru wa kifedha kwa kupata pesa tu, wengi wetu tuna ujuzi ambao tumeupata kutoka shuleni ambao unatuwezesha kupata pesa, tumetumia miaka mingi kupata ujuzi huu na hatimaye tukapata kazi.

Kupata kazi ambayo inaingiza mshahara ni hatua moja bora na ya msingi sana ya kuelekea uhuru wa kifedha ila ni hatua ya kwanza kabisa bado kuna hatua mbili ambazo unatakiwa kuzichukua

## MFANO WA MKULIMA.

Wengi wetu tunategemea chakula ambacho kinazalishwa na wakulima ili kuishi, ila mkulima huwa anapitia hatua zote tatu ambazo nimezitaja hapo juu, unaweza kuwa na mbegu nyumbani kwako (nafaka) ila hii mbegu kama hauizalishi basi haiwezi kukua, kitendo cha kuwa na mbegu na ukaitumia kinakufanya uwe mtegemezi kila siku wa yule mtu ambaye anatoa mbegu ila ukitaka uhuru lazima ujifunze kuzalisha mbegu iliyo mkononi mwako.

Pesa ni kama mbegu unaweza kuwa unaipokea kila siku au kila mwezi kupitia mshahara ila kama kila pesa ikija unaitumia tu bila kuizalisha itakubidi kumtegemea yule anayekupa pesa kila mwezi na huu sio uhuru wa kifedha ukitaka uhuru wa kifedha lazima ujifunze kuwa mkulima wa pesa na hapa nina maana unatakiwa kujifunza kuzalisha pesa

## MFANO WA 2

Miaka kadhaa iliyopita nilikuwa na changamoto sana ya kifedha ijapokuwa pesa nilikuwa Napata nikajiuliza kwa nini siku zote niwe na changamoto ya pesa na jibu nililopata ni kuwa najua kupata pesa ila sijajua jinsi ya kuzalisha pesa kwani pesa inaongezeka pale tu ambapo unajua kuizalisha.

Jaribu kufikiria mfano leo hii una million 1 ni kivipi unaweza kuibadilisha hii milioni 1 kuwa milioni 10? Hapa utahitaji ujuzi wa kuzalisha pesa, na kivipi nikikwambia katika kurasa chache zijazo utakuwa umejifuza kuzalisha pesa?

Kama unataka kutoka hatua ya kwanza ya kupata pesa basi nikukaribishe katika ulimwengu wa uwekezaji na ninakuahidi ya kuwa baada ya kusoma kitabu hiki utakuwa tayari na uwezo wa kuzalisha pesa.

## KOZI FUPI YA UWEKEZAJI.

Ukitaka kuzalisha pesa kama alivyo mkulima itakubidi kujifunza namna ya kulima na kupanda mbegu au unaweza kuwa na pesa ukamwajiri mtu kwa ajili kulima kwa ajili yako,

Sasa katika uzalishaji wa pesa kuna aina mbili za kuzalisha pesa

1) Kuzalisha mwenyewe pesa
2) Kumpa mtu mwenye ujuzi akuzalishie

Sasa njia ya kwanza inaweza kukuchukua muda mrefu sana mpaka kuwa na ujuzi wa kuwekeza kwa faida mfano ukitaka kuwekeza soko la hisa lazima itakubidi kujifunza mengi kama namna soko la hisa linavyofanya kazi na jinsi ya kuchagua kampuni, ila kuna njia ya pili ambayo ndio tutakayoizungumzia hapa kwamba kuna kampuni ambayo iko chini ya umiliki wa serikali chini ya mizara ya fedha ambayo kazi yake kubwa ni kuwekeza kwa ajili yako, hilo halitoshi kampuni hii iko chini ya uangalizi wa benki ya CRDB na imekuwa ikifanya kazi kwa miaka 17 ikiwekeza pesa kwa niaba ya wawekezaji, unachohitaji ni kuwa na pesa na hapa unaweza kuanza kuwekeza hata kama una 5000/= na ukaanza kupata faida za uwekezaji,

Unaweza kuuliza vipi siwezi kupoteza pesa yangu huku? Jibu ni hapana kwani kampuni hii inawekeza katika maeneo salama na kama bado una wasi wasi ni kuwa mpaka sasa hivi kampuni hii inawekeza pesa zaidi ya BILIONI 600, nikutoe shaka kuwa kampuni hii ni salama, na mpaka mwisho wa kitabu utakuwa umejifunza mengi kuhusu uendeshaji wa hii kampuni na usalama wake.

Kama utahitaji pesa yako kwa wakati wowote basi utaipata ndani ya siku kumi za kazi au siku tatu za kazi kwa baadhi ya mifuko.

## ANGALIZO

Kama unataka utajili wa haraka basi kitabu hiki hakiwezi kukufaa kabisa

## KUWEKA AKIBA VS KUWEKEZA

Kuna utamaduni ambao tunafundishwa wa kuweka akiba, ila kuweka akiba sio kuzalisha pesa, unapopata mbegu ukaihifadhi kwa ajili ya matumizi ya baadae wewe una hekima kuliko mtu ambaye haweki akiba kwani kipindi kijacho wewe utakuwa na mbegu na yeye atakuwa hana, ila akitokea mtu ambaye anazalisha mbegu zake anakuwa bora kuliko wewe uliyeweka akiba.

Ukiwa na laki moja ukaiweka ndani mwaka mzima wewe una nidhamu ya fedha na unastahili pongezi ila kama mwenzako akichukua pesa akaiwekeza kwa 12% kwa mwaka ina maana mwisho wa mwaka yeye atakuwa na 112000/= wakati wewe uliyeweka akiba utakuwa na 100000/=.

Kama ulikuwa na milioni 10 mwaka 2005 wakati UTT AMIS inaanza kuwekeza pesa kwa niaba ya wawekezaji na ukaiweka akiba basi leo hii utakuwa na 10 milioni ile ile ila kama uliiwekeza katika mfuko wa UMOJA basi leo hii ungekuwa na zaidi ya milion 120, (milioni mia moja na ishrini) nadhani umeona tofauti kati ya kuweka akiba na kuwekeza.

## NIKIWEKA HELA BENKI JE?

Kuna mtu akasema nikiweka hela benki si ni bora kuliko kuwekeza huko UTT AMIS kwani huku benki nitapokea riba, nikamwambia benki riba unayopokea kwa akaunti ya kawaida ni kati ya 2% mpaka 3% kwa mwaka (hapa ina maana kama umewekeza 100000/= basi utapokea 3000/= kama riba) ila huku UTT AMIS unaweza kupata riba ya 12% mpaka 20% kwa baadhi ya mifuko na kwa baadhi ya miaka (ijapokuwa riba hii huwa inabadilika kutegemea na hali ya

uchumi), na hali ya usalama wa pesa yako huku UTT AMIS haina utofauti sana na benki.

## SEHEMU SAHIHI YA KUZALISHA PESA YAKO.

Sehemu sahihi ya kuwekeza pesa yako lazima iwe na sifa kuu zifuatazo

1) Usalama wa mtaji wako
2) Mrejesho shindani
3) Ukwasi (urahisi wa kupata pesa yako)

## USALAMA WA MTAJI WAKO

Kitu cha kwanza cha kuhakikisha kabla haujaweka pesa yeko sehemu yoyote ile ni usalama wa hilo eneo, itakuwa kitu ambacho sio cha busara umetafuta hela kwa jasho na unaenda kuipoteza kwa kuwekeza sehemu ambayo haina usalama, ninajua watu wengi ambao wamepoteza pesa zao kwa kuwekeza katika kampuni za wizi (scam).

## MREJESHO SHINDANI

Baada ya kuhakikisha kuwa eneo hilo ni salama na unaweza kuwekeza, kitu cha pili ni faida (je faida ni kiasi gani?) sio kitu cha busara kuweka pesa yako sehemu ambayo inatoa riba ya 1% au 2% wakati kuna maeneo unaweza kupata riba mpaka 12% kwa mwaka na kuna usalama.

**UKWASI WA UWEKEZAJI**

Kitu cha mwisho ni kuangalia urahisi wa namna pesa yako (mtaji na faida) ambavyo inaweza kukufikia, kuna maeneo ambayo ukiwekeza japo faida ipo ila sio rahisi kutoa pesa yako endapo unataka kutoa fedha yako, mfano kuna watu waliwekeza katika hisa na mwisho wa siku walipotaka kuuza hisa zao kukawa hakuna mteja wa kununua na ikawa shida kwao kupata pesa zao kwa wakati.

Uwekezaji ambao tunauzungumzia hapa una sifa zote hizi